

## Uchunguzi Linganishi wa Kirai na Neno Ambatani katika Kiswahili

*Adventina Buberwa*  
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania*

### **Ikisiri**

Kirai ni kipashio cha kisintaksia ilhali neno ambatani ni kipashio cha kimofolojia. Vipashio hivi vya nyanja mbili zinazohusiana vimekuwa vikijadiliwa na baadhi ya wanaisimu kwa mitazamo tofautitofauti. Vipashio hivi hutazamwa kama vipashio tofauti na wakati mwingine hutazamwa kama vipashio vinavyohusiana. McCarthy (2002) anadai kwamba neno ambatani ni kipashio kidogo zaidi ya kirai na kwamba kipashio hicho hubebwa na muundo wa ndani wa kirai. Hata hivyo, anasisitiza kwamba kisintaksia neno ambatani hufanya kazi kama neno na siyo kirai. Kwa upande mwingine, Gichuru (2010) anadai kwamba uhusiano wa maneno yanayounda neno ambatani unashabihiana na uhusiano unaopatikana katika miundo ya kisintaksia kama kirai. Madai haya ndiyo yaliyosababisha raghba ya mwandishi kushughulikia uchunguzi linganishi wa vipashio hivyo. Hivyo basi, makala haya yamelinganisha na kulinganua vipashio hivyo kwa kuzingatia muundo, maana, matamshi, uhusiano wa vijenzi na othografia ya vipashio husika.

*Maneno Makuu: Kirai, Neno Ambatani, Neno Kuu*

### **Utangulizi**

Istilahi 'kirai' imefasiliwa na wataalamu mbalimbali wa isimu. Wanaisimu hao wamekuwa wakikitazama kirai kama kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja wanapofasili istilahi hiyo ilhali wakipinga fasili zao kwa ufafanuzi kuwa kirai ni kipashio chenye muundo wa neno moja au zaidi katika uchanganuzi wa miundo yake. Massamba (2004) na Radford (2004), kwa mfano, wanafasili kirai kuwa ni kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja lakini hakina muundo wa kiima na kiarifu. Fasili hii inafanana sana na ile ya Massamba na wenzie (1999) inayodokeza kuwa kirai ni kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja lakini ambacho hakina muundo wa kiima-kiarifu. Aidha, baadhi ya wanaisimu hukirejelea kirai kama kikundi cha maneno (Matei, 2008). Dhana hii pia hudokeza suala zima la kirai kuundwa na kundi fulani la maneno.

Licha ya wataalamu hawa kuzingatia kirai kama kipashio chenye zaidi ya neno moja, uchanganuzi wa virai vilivyohusishwa unabainisha kwamba kirai kinaweza

kuundwa na neno moja. Kwa mfano, Massamba na wenzie (1999) wanapojadili kuhusu kirai nomino wanatoa mifano ifuatayo:

- i. *Chaki* zimekwisha
- ii. *Dada* ameondoka
- iii. *Juma* atarudi kesho

Chanzo: Massamba na wenzie (1999:87)

Nomino ambazo zimeandikwa kwa hati mlalo zinatajwa kuwa mifano ya virai nomino. Katika mazingira hayo ni wazi kuwa mfano huu unapingana na fasili iliyotolewa awali. Dosari kama hii pia inajitokeza katika kitabu cha Matei (2008: 228). Katika mazingira haya ni vigumu kuelewa kama kirai huundwa na ama neno moja au neno moja au zaidi. Hivyo basi, msingi wa fasili za istilahi hiyo muhimu unahitaji kutazamwa upya ili kupata ufafanuzi unaojitosheleza.

Kwa kuwa lengo la makala haya siyo kuangazia ufasaha wa fasili ya kirai, makala haya yatazingatia kuwa kirai ni kipashio chenye maneno mawili au zaidi ili kuweza kufanya uchanganuzi linganishi uliokusudiwa. Hivyo, madai kwamba kirai kinaweza kuwa neno moja hayatazingatiwa katika makala haya.

Kwa upande mwingine, wanaisimu kadha wa kadha wamefasili dhana ya neno ambatani. Kwa mfano, Beuer (1983), Katamba (1993) na Mdee (1997) wanafasili neno ambatani kuwa ni nenounde linalotokana na kuunganisha maneno mawili au zaidi ambayo kwingineko yanaweza kusimama kama neno kamili. Kwa kuzingatia fasili hii ni wazi kuwa neno ambatani huundwa na vipashio viwili au zaidi. Vivyo hivyo, kirai kinajengwa na maneno mawili au zaidi. Katika mazingira haya ni vyema kuchunguza kwa kina kufanana na kutofautiana kwa vipengele hivi muhimu vya lugha ya Kiswahili. Hivyo basi, makala haya yanaangazia suala hili kwa kuzingatia muundo, maana, matamshi na othografia ya vipashio hivyo.

### **Muundo wa Kirai na Neno Ambatani**

Muundo wa kirai na neno ambatani umedokezwa awali katika sehemu ya utangulizi wa makala haya. Kirai katika lugha ya Kiswahili kinaweza kuundwa na maneno mawili au zaidi. Muundo katika mfano 1 inawakilisha baadhi ya miundo ya kirai cha Kiswahili:

#### **Mfano: 1**

- i. Muundo wa Kirai Nomino (Nomino na Kivumishi)**
  - a. Mtu mnene
  - b. Mtoto mtundu
- ii. Muundo wa Kirai Kitenzi (Kitenzi na Nomino)**
  - a. Ameandika barua
  - b. Nimekata mti
- iii. Muundo wa Kirai Kielezi (Kielezi na Kielezi)**
  - a. Haraka sana
  - b. Mbali sana

Mifano hii inadhahirisha kwamba kirai cha Kiswahili kinaweza kuundwa na maneno mawili kama fasili zinavyodokeza. Kwa upande wa neno ambatani, vijenzi vyake pia vinaweza kuwa viwili au zaidi. Chunguza miundo ifuatayo:

**Mfano: 2**

- i. **Muundo wa Nomino na Kivumishi**
  - a. Mwana haramu
  - b. Jua kali
- ii. **Muundo wa Kitenzi na Nomino**
  - a. Chemsha bongo
  - b. Mpiga mbizi
- iii. **Muundo wa Kielezi na Kielezi**
  - a. Kaskazini mashariki

Kwa kuzingatia miundo ya msingi iliyoorodheshwa katika mifano namba 1 na 2 ni vigumu kubaini tofauti za kimuundo baina ya kirai na neno ambatani. Hii ina maana kwamba idadi ya vipashio vinavyounda kirai na neno ambatani inaelekea kufanana. Aidha, suala la vijenzi vyenyewe; yaani aina za maneno zinazoambatana kujenga kirai au neno ambatani vinaonekana kutokutofautiana. Kwa msingi huo, muundo wa kirai na neno ambatani kwa msingi wa idadi na aina ya vijenzi vyake hautofautiani. Hivyo basi, kipengele hiki hakiwezi kudhahirisha tofauti iliyopo kati ya kirai na neno ambatani la Kiswahili. Sehemu inayofuata inaangazia dhana ya neno kuu katika muundo wa kirai na neno ambatani la Kiswahili.

**Dhana ya Neno Kuu katika Muundo wa Kirai na Neno Ambatani**

Dhana ya neno kuu inahusishwa na kirai katika mazingira ya uundaji wa kirai cha aina yoyote. Massamba na wenzie (1999) wanafafanua kuwa kirai huundwa kutokana na mahusiano maalumu na ya asili baina ya maneno. Mahusiano hayo hubainisha kuwa uundaji wa kirai chochote umekitwa katika neno kuu. Aidha, aina ya neno ambalo hutambulika kama neno kuu huwa ni msingi wa kuainisha virai. Tuchunguze mifano ifuatayo:

**Mfano: 3**

- i. *Mtoto* mzuri (kirai nomino)
- ii. *Anakimbia* sana (kirai kitenzi)
- iii. *Mzuri* sana (kirai kivumishi)

Maneno yaliyoandikwa kwa hati mlalo katika mfano wa 3 hapo juu hujulikana kama maneno makuu. Maneno haya ndiyo msingi wa uainishaji wa virai. Kipengele (i) neno '*mtoto*' ni nomino na ni neno kuu katika kirai nomino ambacho kimeundwa na nomino na kivumishi. Katika kipengele (ii) neno '*anakimbia*' ni kitenzi na ni neno kuu katika kirai kitenzi ambacho kimeundwa na kitenzi na kielezi. Kwa upande wa kipengele (iii) neno '*mzuri*' ni kivumishi na ni neno kuu katika kirai kivumishi ambacho kimeundwa na kivumishi na kielezi. Kama mifano hii inavyoonekana, neno kuu katika kirai cha Kiswahili hutokea likiwa neno la kwanza kushoto katika mpangilio wa maneno kadhaa yanavyounda kirai husika.

Ama kuhusu dhana ya neno kuu katika muundo wa neno ambatani haitofautiani na mtazamo wa neno kuu katika muundo wa kirai. Katamba (1993), Kihore na wenzie (2003) na Dressler (2006) wanaeleza kuwa neno ambatani huainishwa kwa kuzingatia kuwepo kwa neno kuu na mahali ambapo neno kuu hutokea katika muundo husika. Anaendelea kueleza kuwa neno kuu katika neno ambatani hutawala neno zima na huathiri maneno mengine katika muundo wake. Uundaji wa neno ambatani kama ulivyo uundaji wa kirai, huzingatia neno kuu. Hivyo, neno kuu la neno ambatani la Kiswahili huwa ni sehemu inayotabiri aina na maana ya neno. Tazama mifano ifuatavyo:

**Mfano: 4**

- i. *Mwalimu* mkuu (aina ya mwalimu)
- ii. *Kiambishi* tamati (aina ya kiambishi)
- iii. *Isimu* jamii (aina ya isimu)

Maneno yaliyoandikwa kwa hati mlalo katika mfano wa 4 ni mifano ya maneno makuu ya maneno ambatani ya Kiswahili. Ni wazi kwamba neno kuu katika kirai na neno ambatani hutokea kushoto kama ilivyokwisha kuelezwa. Aidha, neno kuu ndio msingi wa kile kinachorejelewa; yaani ukitaja ‘mwalimu mkuu’ kirejelewa ni aina ya ‘mwalimu’ na siyo aina ya ‘mkuu’. Kwa kuzingatia ufafanuzi huu na mifano kuntu iliyowasilishwa ni dhahiri kwamba kirai na neno ambatani la Kiswahili haviwezi kutofautishwa kwa msingi wa neno kuu.

**Maana katika Muundo wa Kirai na Neno Ambatani**

Maana inatajwa na baadhi ya wanaisimu kuwa kigezo kinachoweza kutofautisha kirai na neno ambatani. McCarthy (2002) anaeleza kwamba neno ambatani hubeba maana ambayo inaweza kutabirika kutokana na maneno yanayojenga mwambatano fulani. Anaendelea kusema kuwa maana ya kirai haitabiriki na maana yake hudokeza taarifa kuhusu jambo fulani na anasisitiza kuwa taarifa itolewayo huwa siyo kamili. Kwa kuzingatia ufafanuzi huu tunaweza kusema kwamba neno ambatani ‘*mwana hewa*’ lina maana ya mtu anayejihusisha na hewa, neno ‘*mwana anga*’ lina maana mtu anayejihusisha na anga ilhali ‘*mwanafunzi bora*’ ni kirai kinachotoa taarifa kuhusu namna mwanafunzi alivyo. Licha ya kutabirika kwa maana ya maneno ambatani yaliyotajwa, na kutokutabirika kwa maana ya kirai, tofauti ya vipashio hivi muhimu inaonekana kuwa telezi. Kirai na neno ambatani vyote hudokeza maana. Kudai kwamba maana au taarifa inayodokezwa na kirai siyo kamilifu siyo hoja muhimu kuhusu kutofautiana kwa vipashio husika kwa sababu kirai huundwa na maneno kamili na maneno hayo sharti yawe na maana. Kwa msingi huo, kutokukamilika kwa taarifa zinazodokezwa na kirai kunaibua dukuduku kwamba ni taarifa zipi nyingine zinatarajiwa kudokezwa na kirai ambacho kimekamilika?

Aidha, Gichuru (2010) anaeleza kwamba neno ambatani hudokeza dhana moja tofauti na kirai. Ili kuthibitisha maelezo haya, tuchunguze mifano ifuatayo:

**Mfano: 5**

- i. Mwana anga (neni ambatani)
- ii. Mwana hewa (neni ambatani)
- iii. Mtoto mrefu (kirai)
- iv. Mwanafunzi mzuri (kirai)

Kama ilivyodokezwa awali, neno ambatani ‘*mwana anga*’ katika mfano (i) ni mtu anayejihusisha na anga. Tukichukua kirai katika mfano (iii) ambacho ni ‘*mtoto mrefu*’ kinadokeza mtoto mwenye sifa ya urefu. Katika mazingira haya dhana zinazodokezwa na vipashio hivi viwili zinaonekana kuwa ni dhana zinazotofautiana kwa sababu maana ya neno ‘*mwana anga*’ siyo jumla ya maana ya maneno hayo kama ilivyo kwa upande wa kirai ‘*mtoto mrefu*’ ingawa maneno makuu katika vipashio vyote yanafanuliwa na maneno yanayoambatana nayo; yaani ‘*anga*’ na ‘*mrefu*’.

Suala la msingi linalotakiwa kuzingatiwa katika kipengele hiki ni kwamba maana za maneno ambatani hutofautiana na maana za virai kutokana na ukweli kwamba maana za virai hutokana na jumla ya maana za maneno yanayounda kirai husika. Maana za maneno ambatani hazitokani na jumla ya maana za maneno yanayounda neno fulani (Mbutu, 2008). Maana za maneno ambatani zinaweza zisidokezwe na maneno (vijenzi) yanayounda neno ambatani. Kwa mfano neno ambatani ‘*kifungua kinywa*’ halina maana ya kufungua mdomo bali linamaanisha chakula cha asubuhi. Tofauti na mfano huo, kirai ‘*anakula chakula*’ kinadokeza maana ya mtu kupata mlo na sivinginevyo. Izingatiwe kuwa neno ambatani hujengwa na maneno mengi kama kirai lakini maneno hayo hufanya kazi kama neno moja lenye maana moja.

**Mkazo katika Muundo wa Kirai na Neno Ambatani**

Mgullu (1999) anafasili mkazo kuwa ni sifa ya utamkaji ambapo mtu hutumia nguvu zaidi katika utamkaji wa sehemu fulani. Katika Kiswahili, mkazo huwekwa katika silabi ya mwisho kasoro moja. McCarthy (2002) anaeleza kuwa mkazo ni kipengele kinachoweza kutofautisha kirai na neno ambatani. Katika Kiswahili, mkazo huwekwa katika silabi ya mwisho kasoro moja ya neno la pili wakati katika kirai cha Kiswahili mkazo huwekwa katika silabi ya mwisho kasoro moja ya neno la kwanza yaani neno kuu. Tazama mifano ifuatayo:

**Mfano: 6**

- i. **Mkazo katika neno ambatani**
  - a. Mwana *’hewa*
  - b. Bata m’*zinga*
- ii. **Mkazo katika kirai**
  - a. Mche *’zaji* bora
  - b. M’*zuri* sana

Silabi zilizoandikwa kwa hati mlalo ndizo zinatamkwa kwa nguvu zaidi ya silabi zingine. Kama mfano 5 unavyoonekana, ni wazi kwamba kigezo cha matamshi kinaweza kutumika kuonesha tofauti kati ya kirai na neno ambatani. Sehemu inayofuata inachunguza totauti za kiothografia kati ya kirai na neno ambatani.

### Othografia ya Kirai na Neno Ambatani

Kipengele hiki kinaangazia namna kirai na neno ambatani zinavyotofautiana au kufanana kimaandishi. Kirai cha Kiswahili huandikwa kwa kuacha nafasi baina ya maneno yanayounda kirai husika. Chunguza mifano ifuatayo:

#### Mfano: 7

- i. Shule kubwa (kirai nomino)
- ii. Mwalimu mzuri (kirai nomino)
- iii. Twende haraka (kirai kitenzi)
- iv. Haraka sana (kirai kielezi)

Kwa upande wa neno ambatani, zipo aina tatu za maumbo yanayojidhihirisha kimaandishi. Maumbo haya ni pamoja na maumbo yasiyounganishwa, maumbo yanayounganishwa na maumbo yanayotengwa kwa kistari. Mifano ifuatayo inashadidia hoja hii:

#### Mfano: 8

- i. Umbo lililounganishwa**
  - a. Mwanamke
  - b. Mwenyekiti
  - c. Isimujamii
- ii. Umbo lisilounganishwa**
  - a. Sarufi zalishi
  - b. Nomino ambatani
  - c. Nomino dhahania
- iii. Umbo linalotengwa kwa kistari**
  - a. Mkondo-hewa
  - b. Lugha ambishi-bainishi
  - c. Tendo-uneni

Kwa kuzingatia mifano iliyoorodheshwa hapo juu, tofauti kati kirai na neno ambatani kimaandishi ni kwamba wakati kirai hujibainisha katika umbo lenye kuacha nafasi baina ya maneno, neno ambatani linaweza kuandikwa ama kwa kuyaunganisha maneno kama katika kipengele cha (i), kwa kuacha nafasi kama katika kipengele cha (ii) au kwa kuyatenganisha maneno kwa kistari kama katika kipengele cha (iii). Kwa hakika ufafanuzi huu uko wazi sana katika kulinganisha na kulinganua vipashio hivi viwili.

### Uhusiano wa Vijenzi vya Kirai na Neno Ambatani

Kipengele hiki kinaangazia uhusiano wa vijenzi vya kirai na neno ambatani katika Kiswahili. Gichuru (2010:91) anadai kwamba vijenzi vya neno ambatani hudhihirisha uhusiano wa kisarufi unaoshabihiana na uhusiano unaopatikana katika miundo ya kisintaksia. Madai haya yanatushawishi kuamini kuwa neno ambatani linaweza kutazamwa kama kipashio cha kisintaksia. Aidha, Gichuru (*keshatajwa*) anabainisha uhusiano wa aina tatu wa vijenzi vya neno ambatani ambao ni *uhusiano vumishi*, *uhusiano tegemezi* na *uhusiano ambatani huru*. Anaendelea kueleza kuwa uhusiano

vumishi hujitokeza pale ambapo neno moja hutoa maelezo zaidi kuhusu neno lingine ambalo kwa pamoja huunda neno ambatani. Mifano ifuatayo inadhahirisha maneno ambatani yenye vijenzi vyenye uhusiano vumishi:

**Mfano: 9**

- i. Mwalimu *mkuu*
- ii. Mjamzito
- iii. Mwana *haramu*

Katika mfano wa 9 hapo juu, maneno yaliyoandikwa kwa hati mlalo yanatoa taarifa au maelezo zaidi kuhusu neno kuu na hivyo uhusiano wake hujulikana kama uhusiano vumishi. Kwa kuzingatia uhusiano huu, vijenzi vya kirai cha Kiswahili pia huwa na uhusiano huo. Tazama mifano ifuatayo:

**Mfano: 10**

- i. Mtoto *mdogo* (kirai nomino)
- ii. Vizuri *sana* (kirai kivumishi)
- iii. Haraka *sana* (kirai kielezi)

Kama ilivyo katika mfano wa 9, maneno makuu katika virai vilivyotakwa katika mfano wa 10 yanafanuliwa na maneno yaliyoandikwa kwa hati mlalo. Katika mazingira haya ni vigumu kutofautisha kirai cha Kiswahili na neno ambatani la Kiswahili.

Kwa upande wa uhusiano tegemezi, Gichuru (keshatajwa) anaeleza kwamba vijenzi vya neno ambatani huwa na uhusiano wa kutegemeana na kukamilishana. Inaelezwa kwamba maneno makuu huwa tegezi kwa maneno yanayofuata. Chunguza mifano hii:

**Mfano: 11**

- i. *Mwendesha* bodaboda
- ii. *Kiruka* njia
- iii. *Kiinua* mgongo

Mifano hii inaonesha kwamba maneno makuu; yaani maneno yaliyoandikwa kwa hati ya mlalo hayawezi kusimama peke yake bila kukamilishwa na vijalizo vyake. Hivyo uhusiano huu unajulikana kama uhusiano tegemezi. Swali la kujiuliza ni kwamba je kuna uhusiano tegemezi baina ya vijenzi vinavyounda kirai? Ukweli ni kwamba vijenzi vya kirai cha Kiswahili hutegemea neno msingi ambalo ni neno kuu. Neno kuu linaweza kuachwa pekee yake likawa na maana. Hivyo basi, maneno yanayoambatana na neno kuu katika kirai hufanya kazi ya kutoa taarifa zaidi kuhusu neno kuu na siyo kulikamilisha neno kuu. Kwa mfano, kirai '*mzuri sana*' likiondolewa neno '*sana*' neno '*mzuri*' hubaki na maana yake ya msingi. Pia, kirai '*haraka sana*' neno '*sana*' likiondolewa neno '*haraka*' hubaki na maana yake ya msingi.

Fauka ya hayo, uhusiano ambatani huru unafanuliwa kuwa ni uhusiano unaojitokeza pale neno ambatani linapoundwa na vijenzi vyenye cheo sawa. Gichuru (2010: 93) amafanua kwamba vijenzi hivyo huwa havitegemeani wala kuvumishana

bali hurejelea vitu tofauti. Mifano ya maneno ambatani yenye vijenzi kama hivyo inayohusishwa na madai haya ni kama ifuatayo:

**Mfano: 12**

- i. Kitenzi *jina*
- ii. Mpiga *taipu*
- iii. Mpiga *mbizi*

Uhusiano wa vijenzi vya maneno ambatani ya mfano huu hautofautiani na ule wa mifano ya maneno ambatani katika mfano wa 10 na 11. Maneno makuu yanategemea vijalizo vyake (maneno yenye hati mlalo) ili kukamilika. Aidha, vjalizo hivyo vinafafanua neno kuu; yaani '*kitenzi jina*' ni kitenzi chenye sifa ya kuwa jina, '*mpiga taipu*' ni mtu anayepiga taipu na '*mpiga mbizi*' ni mtu anayepiga mbizi. Kwa kuzingatia mjadala huu na mifano kuntu iliyotolewa chini ya kipengele hiki, ni dhahiri kuwa uhusiano wa vijenzi vya kirai na neno ambatani hufanana kwa namna moja na kutofautiana kwa namna fulani. Vijenzi vya neno ambatani huwa na uhusiano tegemezi na uhusiano vumishi ilhali vijenzi vya kirai huwa na uhusiano vumishi pekee.

**Hitimisho**

Makala haya yameangazia kufanana na kutofautiana kwa kirai na neno ambatani la Kiswahili. Mjadala uliowasilishwa katika makala haya unadhahirisha kwamba kuna uhusiano baina ya kirai na neno ambatani. Imedhahirika kwamba ni vigumu kutofautisha kirai na neno ambatani kwa kuzingatia muundo wake; yaani idadi na aina ya vipashio vinavyounda kategoria hizo. Aidha, imeonekana kwamba kigezo cha maana pia ni telezi katika kufanua tofauti ya kirai na neno ambatani. Imesisitizwa kuwa huenda utelezi huo unatokana na dhana yenyewe ya maana kuwa telezi. Hata hivyo, imebainika kwamba mkazo unaweza kutumika kubaini tofauti kati ya kirai na neno ambatani la Kiswahili. Zaidi ya hayo, uhusiano wa vijenzi vya vipashio hivyo unaonekana kufanana hususani kwa upande wa uhusiano vumishi. Kwa hakika vipashio hivi vinahusiana zaidi kuliko kutofautiana. Hoja hii haitashangaza kwa namna yoyote kwa sababu nyanja zote za isimu huhusiana na kutofautiana. Kwa msingi huo huenda vipashio hivi vinahusiana kwa sababu kuna uhusiano kati ya nyanja za mofolojia na sintaksia.



**Marejeo**

- Beuer, L. (1983). *English Word Formation*. Cambridge University Press.
- Dressler, W. (2006). 'Compound Types' katika Libben na Jerema (wahariri): *The Representation and Processing of Compound Words*. Oxford: Oxford University Press.
- Gichuru, T. M. (2010). Uchanganuzi wa Nomino Ambatani za Kiswahili: Mtazamo wa Mofolojia Leksika. Tasnifu ya Umahiri, haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.
- Katamba, F. (1993). *Morphology*. New York: Palgrave.
- Kihore, Y.M, Massamba, D.P.B. na Msanjila, Y.P. (2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu: Sekondari na Vyu*. Dar es Salaam: TUKI.
- McCarthy, A. (2002). *An Introduction to English Morphology: Words and their Structure*. Edinburgh: Edinburg University Press.
- Mdee, J.S. (1997). *Nadharia na Historia ya Leksikografia*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mgullu, R. S. (1999). *Mtaala wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Massamba, D.P.B. (2004). *Kamusi ya Falsafa na Isimu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Massamba, D.P.B. (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili: Sekondari na Vyu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Matei, A. (2008). *Darubini ya Sarufi: Ufafanuzi Kamili wa Sarufi*. Nairobi: Phoenix Publisher.
- Radford, A. (2004). *English Syntax: An Introduction*. Cambridge: Cambridge University Press.

